JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MANYUNYU,
S.L.P. 619,
NJOMBE

28 / 03 / 2022

KUMB. Na MGSS/ FV/ RFG / VOL. 1/ 09
NDUGU ……
MZAZI / MLEZI WA ……
S. L. P……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANYUNYU, HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE, MKOA WA NJOMBE MWAKA 2022

- Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya …….. Shule ya Sekondari Manyunyu ipo umbali wa kilomita 54 Mashariki mwa Mji wa Njombe. Usafiri Mjini Njombe wa basi unapatikana katika kituo cha Mabasi yanayoanzia stendi kuu Njombe na Kibena Madukani. Muhula wa masomo unaanza mwezi Julai hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ***……..*** Kama atakuwa hajaripoti baada ya kufungua shule nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. Mwanao anatakiwa aje na **photocopy** ya cheti cha kuzaliwa pamoja na cheti kinachoonyesha matokeo yake ya kidato cha nne (**photocopy)** kwa ajili ya usajili moja ya kila cheti.
- Shule hii ipo katika mazingira mazuri ya kujifunza na kusomea, majengo mazuri, maji na umeme wa kuaminika. Ni matumaini yangu kuwa utasoma maelezo yaliyoambatanishwa ili uweze kushirikiana na uongozi wa shule katika kufuatilia maendeleo ya mwanao kitaaluma na kinidhamu. Jaza fomu zilizoambatanishwa na ziwasilishe shuleni wakati wa kuripoti.
- KAULI MBIU YA SHULE ‘’ SCHOOL MOTTO’’ NI: “ELIMU IMKOMBOE MWANAMKE” (EDUCATION SHOULD LIBERATE A WOMAN).

Kauli hiyo ndio dira yake kwa muda wote atakapokuwa hapa shuleni hivyo atatakiwa kuitafakari kwa vitendo.

Ni matumaini yetu kuwa atatumia fursa hii kusoma kwa bidii kwa manufaa yake na Taifa kwa ujumla

MAWASILIANO:

- **MKUU WA SHULE 0752 – 282394**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE: 0764 – 988373**
- **.. MWALIMU WA MALEZI: 0713 – 996936 / 0764 – 983747**

1. SARE ZA SHULE

- Blauzi 2 nyeupe tetron mikono mirefu
- Sketi 2 za darasani ziwe ndefu na tai 2 rangi ya chungwa rinda box anaweza kushona shuleni kama imeshindikana huko. (*kitambaa kimeambatanishwa*)
- Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba jozi 2 **visiwe na visigino virefu.**
- Sweta zito rangi ya bluu la uzi lisiwe na alama yoyote, shingo **V.**
- Soksi nyeupe jozi 2 zisiwe na alama yoyote
- T - shirt rangi ya kijivu yenye nembo ya shule anaweza kupata shuleni.
- Hijabu rangi nyeupe isiyo na urembo wowote (***kwa wanafunzi wa kiislamu***)
- T- shirt rangi ya blue anaweza kupata shuleni
- Track suit rangi ya kijivu yenye mistari myeupe anaweza kupata shuleni kama itaikosa huko.
- Vazi la kazi (gauni) mshono solo linaweza kushonwa shuleni kitambaa draft nyeupe na nyekundu. (*kitambaa kimeambatanishwa*)
- Sketi fupi ya michezo (mshono solo) urefu usawa wa goti na Bukta rangi ya damu ya mzee zinaweza kushonwa shuleni*. (kitambaa kimeambatanishwa)*
- Raba za michezo nyeupe
- Pullneck nyeupe moja (01)

2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

- Ada ya shule ……. 70,000/= kwa mwaka (35,000/= kwa muhula)
- Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi / mlezi.

- Ukarabati ……..15,000/=
- Kitambulisho na picha …… 6,000/=
- Taaluma …… 20,000/=
- Dawati na kiti ……20,000/=
- Walinzi, wapishi na vibarua wengine ….. 30,000/=
- Nembo ya shule …… 2,000/=
- Matibabu (huduma ya kwanza) … 5000/=
- Tahadhari …… 10,000/ = (haitarudishwa)
- Mitihani ya ndani ……10,000/=

JUMLA YA ADA NA MICHANGO KWA MWANAFUNZI NI = **188,000/=**

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule (Account No**. 60606600124 NMB)** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip.)

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni.

- RIMU A_4 500g**.** 1 kwa mwaka.
- Scientific calculator
- Godoro la ft **$2^1/_2$** unene inchi ‘’6’’.
- Laboratory coat kwa wanafunzi wa PCB

- Blanketi zito 1, mashuka mawili (2) rangi nyeupe (yasiwe na maua)
- Mto na foronya 1 rangi nyeupe
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- Ndoo ndogo mbili (02) lita 10
- Daftari na kalamu za kutosha
- Mwenye kadi ya Bima ya Afya aje nayo.
- Rula na mkebe wenye vifaa vyote
- Mswaki, dawa ya mswaki na sabuni za kutosha
- Tochi,mwavuli, taulo, kanga doti 2, toilet paper (TP), taulo za kike (pads) na nguo za ndani za kutosha.
- Begi la kubebea madaftari.

(d) Vifaa vya usafi

- PCB waje na jembe 01 lenye mpini na reki 01
- HGL na HGK waje na jembe 01 lenye mpini na slesha 01
- HKL waje na shoka 01 lenye mpini

Vitabu vya masomo angalia orodha iliyoambatanishwa kwa kila somo. Unaweza kununua baadhi ya hivyo au vingine vinavyopatikana vyenye ubora.

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ utoro
- Kugoma na kuhamasisha mgomo
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule
- Kusuka nywele
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- Uvutaji wa sigara
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
- Kupata ujauzito au kutoa mimba
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau bendera ya Taifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

MAELEKEZO MUHIMU

- Vifaa vya muziki haviruhusiwi
- Usifike bwenini bila kuripoti ofisini
- Usije na kifaa chochote kinachotumia umeme mf. Pasi, heater, birika linalotumia umeme
- Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule haziruhusiwi
- Kuwa na nywele ndefu au kuweka dawa hairuhusiwi
- Ni marufuku kuja na kofia /mzula, pete, rangi za vidole na midomo.
- Masanduku makubwa hayaruhusiwi, kwani hakuna nafasi ya kuyaweka bwenini.
- Kuwa na heshima
- Kuhudhuria ‘’assemble’’ wakati wote inapobidi
- Kuhudhuria darasani kulingana na ratiba za vipindi na kwenye mikutano yote halali.
- Wanafunzi wote wanatakiwa kujisomea usiku (prep) kulingana na ratiba ya shule.
- Wanafunzi wanatakiwa wavae sare zinazokubalika na uongozi wa shule wakati wa masomo darasani, wanapokwenda makwao wakati wa likizo na wanaporudi shule baada ya likizo
- .Wanafunzi hawatakiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu.
- Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia nyumba za walimu na watumishi wasio walimu, ofisi ya shule, maabara na jikoni bila ruhusa maalumu
- Usafi wa mwili na mazingira
- Mwanafunzi haruhusiwi kugoma au kukataa uongozi pindi anapochaguliwa au kuteuliwa.
- Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na hela bwenini zaidi ya sh. 5000/= (fedha za matumizi zaidi ya sh. 5000/= zitatunzwa kwa Mhasibu.

18. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula wala kinywaji chochote shuleni Mwisho wa kupokelewa mwanafunzi ni saa kumi na mbili kamili jioni (12:00).

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja Manyunyu Sekondari

*Karibu sana**!***

_____

ADVERA J. BAGOKA

MKUU WA SHULE

Nakala kwa

1. Katibu Mkuu,
OWM – TAMISEMI,
S. L.P.
DODOMA

2. Mkaguzi Mkuu wa Kanda,
S.L.P.2288,
Iringa.

3. Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Njombe,
S.L.P. 547,
NJOMBE.

B. FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI

I: MWANAFUNZI

- Mimi …….. kidato cha ……..
- Nakubali kujiunga na shule hii ya Sekondari Manyunyu nikiwa mwanafunzi wa Bweni / Hosteli.
- Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote, sheria na taratibu zote za shule. Nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya Sekondari Manyunyu.
- Kwa hiyo naahidi kwamba:-
    - Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
    - Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vita kuwa kinyume na uongozi wa Chama Tawala na Serikali ya Jamhuri ya Muunganowa Tanzania.
    - Nitatunza Mali ya Umma ambayo ni pamoja na mazingira, samani (funiture), vitabu n.k.
    - Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu
    - Nitashiriki katika shughuli zingine mbali na masomo ya darasani.

Saini ya mwanafunzi …….. tarehe …….

II: MZAZI/ MLEZI

Mimi …….. Ninakubali mtoto wangu
…….. Kidato cha …….. mwaka 20……..
Tarehe…….. akiwa mwanafunzi wa Bweni/ Hostel

Kwa hiyo naahidi:-

- Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule walimu na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu
- Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulu kwa muda wote awapo shuleni.
- Anwani yangu ya kudumu ni ……
  ……

Saini ya mzazi / mlezi …….. tarehe……..

B.III. KUWATEMBELEA WANAFUNZI / SIKU YA WAGENI

Wazazi / walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa mwezi ambayo ni kila Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 10:30 jioni. Mwalimu wa zamu atakuwepo shuleni kwa muda huo kupokea wageni; hairuhusiwi kumletea mwanafunzi chakula.

C. FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI MWANAFUNZI

- Jina kamili ……..
- Mahali ulipozaliwa ……
- Tarehe ya kuzaliwa ……..
- Uraia ……
- Anwani ya nyumbani ……..
- Anwani ya mzazi / mlezi (kama tofauti na hiyo hapo juu) …….
- Jina la mzazi / mlezi ……

Ndugu wa karibu 4 watakaoruhusiwa kuja kumwona mwanafunzi akiwa shuleni.

Na	JINA KAMILI	UHUSIANO	ANWANI	SIMU

8. Dini ……
9. Kidato unachopokelewa ……..
10. Shule unayotoka ……..
11. Shughuli unayopendelea mbali na masomo ya darasani kama vile mpira wa pete, riadha, kuimba n.k. ……
12. Wilaya unayotoka …… Mtaa ……. Kata……..

    N.B.

    Hutaruhusiwa kubadili dini, dhehebu bila uthibitisho wa barua kutoka kwa mzazi au mlezi. Barua ipitishwe na mtendaji kata unakotoka.

13. Saini ya:

Mwanafunzi …….. tarehe ……
Mzazi/mlezi ……..tarehe ……..

MATUMIZI YA OFISI TU:

Namba ya shule ……
Namba ya mtihani ……



D. FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

MANYUNYU SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 619,
NJOMBE.

THE MEDICAL OFFICER:
……..
……..
……..

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Kindly please examine …….. to determine her physical and mental fitness for pursuing secondary school studies.

- Eyesight .....
- Hearing……
- Spleen……
- Limbs……
- Epilepsy……
- Cardiac disease……..
- Venereal diseases……
- Rheumatism……
- Pregnancy……..
- Any other serious diseases ……
- General comments …….....

……
……

_____

ADVERA J. BAGOKA
MKUU WA SHULE

STAMP ……

E. ORODHA NA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

A. HISTORY

- Modern word History by Ben Warsh
- Africa in the world History by Nyirenda
- The Russian Revolution and the Bolshevik
- Major events in the Africa History by Fr. Kamara
- Zamani East Africa History by Ogot and J.A Kieban

B. KISWAHILI.

- Kunga za fasihi na lugha (Msokile m. 1992) EDP
- Historia ya Kiswahili Africa Mashariki (Shiragdin na Mnyapala)
- Kunga za ushairi na Diwani yetu (Mlokozi M. na Mnyapala)
- Sarufi ya Kiswahili sekondari na vyuo (Mdee) DUP – DSM
- Ndimi na Hisia za wabakiki katika kioo cha lugha - DSM (Senkoro 1973)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu – TUKI

C. GEOGRAPHY

- Principles of physical Geography by F. J. Monkhouse
- General Geography in diagram by R. B. Burnet
- Simplified physical Geography (A level) by D. M. Mapunda
- Statistical methods and the Geography by S. Gregory
- Certified physical and human Geography by Goh Chang Leong
- Geography an integrated Approach by Goh Chang Leong

D. ENGLISH

- English for Advanced level by Dr. Kadeghe
- Advanced English Dictionary – Oxford University
- Selected poems from East Africa by Institute of Education and other poems text books
- I will marry when I want by Ngugi wa Thiongo and other plays / drama text books
- His Excellency. The head of state by Danny Safo and other novels short stories books

E.PHYSICS

- Advanced Level Physics (4^{th} Edition) (1993) by Muncaster
- Principle of Physics for Class XII (2007) By Mehta, V.K& Mehta R.
- Advanced Physics (5^{th} Edition). (2000) By Duncan, T.

F. CHEMISTRY

- Conceptual chemistry for class XI by Dr. S. K. Jain (S. Chand)
- Advanced Chemistry Review 1 & 2 (2004), by William W. Davis (Mzumbe bookshop project)
- Physical chemistry (1998), by Delungu, et al. (Mzumbe bookshop project)

G. BIOLOGY

- Biological science third by D.J. Taylor, N.P.O Green and G.W. Stout
- Advanced biology principle and application by CJ Clegg and DG McKean.
- New understanding biology for advanced level by Glenn and Susan Toole
- Plant and animal biology volume 1& 2 by AE vines and N Rees.
- Biology for class XI & XII by Dr. P.S. Verma and Dr. B.P. Pandey.

H. GENERAL STUDIES

1. Advanced level general studies notes form 5 & 6 by Nyambari Nyangwine 2009.
2. General studies for advanced level certificate form 5 & 6 by Richard R.F. Mbalase.

N.B. Mwanafunzi anaweza kuwa na kitabu kimoja au zaidi kwa kila somo kulingana na tahasusi/mchepuo wake.

KARIBU SANA MANYUNYU SEKONDARI!!

Saini ya Mkuu wa shule ……..

Jina la Mkuu wa shule ……..

Muhuri wa Mkuu wa shule ……..